**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MWANZA - MWANZACOHAS**


Phone: +255 28 2500239
Fax No**:** 255 28 2500501
Email**:**principal@mwanzacohas.ac.tz

MWANZACOHAS
P. O BOX 476
**MWANZA**

01/07/2026

**Kumb: …………………………………...**

**Kwa……………………………………….**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA HEALTH INFORMATION SCIENCES (HIS) KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya **HEALTH INFORMATION SCIENCES (HIS)** ngazi ya Nne (NTA Level 4) katika Chuo cha **MWANZACOHAS** Mafunzo haya ni ya miaka mitatu (3).

Chuo kitafunguliwa tarehe **19.OCTOBA 2026** na unapaswa kuripoti chuoni kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 11.30 jioni. Endapo utashindwa kuripoti ndani ya wiki mbili (2) tangu chuo kufunguliwa nafasi yako itapotea na kujazwa na muombaji mwingine.

Ili kukamilisha usajili na kupokelewa chuoni unatakiwa kufanya yafuatayo: -

i) Kukamilisha malipo ya ada kama ilivyoainishwa katika majedwali ya gharama za mafunzo hapo chini (*Sehemu A*). Malipo haya yatafanyika kupitia benki na mitandao ya simu kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** utakayopewa kabla ya kuwasili chuoni. Ili kupata namba ya kumbukumbu ya malipo, tafadhali wasiliana na **Mhasibu wa Chuo** kupitia namba ya simu **0755-680-053 au afisa udahili 0757400555** Mwanafunzi ambaye hatalipa ada iliyoainishwa kwenye kipengele hicho hatapokelewa.

ii) Pima afya yako katika hospitali (**sio zahanati/kituo cha afya**) inayotambulika na kujaziwa Fomu ya Matibabu (Medical Examination Form) kabla ya kuripoti chuoni.

iii) Kujaza Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo utakayopewa ufikapo chuoni. Unakumbushwa kuzisoma na kuzielewa sheria zote kabla ya kusaini.

iv) Kujaza Fomu iliyoambatishwa hapo chini inayohusu Taarifa za Wazazi/Walezi wako

v) Kununua vifaa vyote vilivyoainishwa katika sehemu B hapo chini vitakavyokuwezesha katika mafunzo yako uwapo chuoni. Hii ni pamoja na sare za chuo.

## SEHEMU A: MAELEKEZO YA MALIPO

Jumla ya fedha itakayolipwa chuoni ni **920,000 (shilingi Laki tisa na ishirini) kama jedwari namba 1 linavyoonyesha.**

Fedha hizi zinajumuisha gharama za mafunzo zinazolipwa chuoni moja kwa moja na gharama zisizo za mafunzo zinazolipwa kwenye mamlaka na Taasisi nyingine za Serikali. Tafadhali kumbuka **FEDHA HIZO ZIKISHALIPWA CHUONI HAZIRUDISHWI (NON-REFUNDABLE).**

kwa mwanafunzi asiye na bima atapaswa kulipa Jumla ya Tsh 50,400.00 kwa mwaka. Na wale wenye bima za afya (zilizo hai) ACTIVE waje na kadi zao zikagulipe katika mfumo.

Mchanganuo wa malipo ni kama ulivyoainishwa katika majedwali yafuatayo:

### I. Gharama zinazolipwa moja kwa moja Chuoni kwa wanafunzi wote NTAL 4:

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatalipwa moja kwa moja chuoni kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number) itakayotolewa **na MHASIBU** . Mwanafunzi anaweza kulipa malipo ya ada ya mwaka mzima kwa mara moja au kwa awamu mbili kama inavyoonekana katika mchanganuo ufuatao:

**Jedwali 1: Gharama zinazolipwa moja kwa moja Chuoni:**

| KIPENGELE | MALIPO MUHULA WA KWANZA | MALIPO MUHULAWA PILI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mafunzo | 200,000.00 | 200,000.00 | 400,000.00 |
| Mitihani ya Ndani | 100,000.00 | - | 100,000.00 |
| Mitihani ya Nje | - | 150,000 | 150,000 |
| Usajili | 20,000.00 | - | 20,000.00 |
| Michezo | 10,000.00 | - | 10,000.00 |
| Fedha ya Dharura | 10,000.00 | - | 10,000.00 |
| Malazi (kwa wanafunzi wa bweni) VYUMBA NI VICHACHE HII NI KWA WALE WENYE MAHITAJI MAALUMU | 150,000.00 | - | 150,000.00 |
| Practicum Guide, Practicum placement fee and Procedure Book | 80,000.00 | - | 80,000.00 |
| **JUMLA** | **570,000.00** | **350,000.00** | **920,000.00** |

**NB: 1.** Malipo tajwa katika Jedwali namba 1, yanapaswa kufanyika kila mwaka wa masomo. Ada ya muhula wa kwanza italipwa yote mara tu unapowasili chuoni na ya muhula wa pili italipwa ndani ya siku 14 baada ya kuanza muhula wa pili.

**2. Wanafunzi kuanzia umri wa miaka 18 na kuendelea , ni lazima wafike na namba zao za NIDA . Chuo hakitahusika na ufuatiliaji wa NIDA.**

**II. Malipo ya Gharama za Quality assurance ( NACTVET) na BIMA ya Afya (NHIF)**

Malipo ya vipengele vifuatavyo yatafanyika pia kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (control number**)** itakayotolewa **NA MAMLAKA HUSIKA**. Ikumbukwe pia kuwa malipo ya vipengele hivi yatafanyika mwanzoni mwa kila mwaka wa masomo.

**Jedwali 2: Malipo ya Gharama za Quality assurance (NACTVET), na BIMA ya Afya (NHIF)**

| KIPENGELE | KIWANGO CHA MALIPO |
|---|---|
| Gharama za Matibabu (kwa wasio na BIMA) | 50,400.00 |
| NACTEVET Quality Assurance | 20,000.00 |
| Gharama za uhakiki wa wanachuo kwenye mfumo wa udahili wa NACTVET (Kwa wanachuo waliochaguliwa na OR-TAMISEMI tu) | 10,000.00 |

**NB:**

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na kadi ya bima ya afya ili imsaidie akapohitaji huduma ya matibabu. Kulipia gharama za matibabu ni jukumu la mzazi. Ili mwanafunzi aweze kusaidiwa kupata kadi ya bima ya afya, mzazi ana wajibu wa kuhakikisha mwanafunzi huyo ana namba ya kitambulisho cha NIDA na kiwango cha fedha kinachotakiwa kwa ajili ya malipo hayo. Namba ya kitambulisho cha NIDA ni muhimu wakati wa usajili wa mwanafunzi katika Huduma za Bima ya Afya.

2. Wanafunzi waliochaguliwa moja kwa moja kupitia OR-TAMISEMI watapaswa kulipia gharama kwa ajili ya uhakiki. Gharama za uhakiki wa wanafunzi zimewekwa na NACTVET ili kuhakiki wanafunzi waliochaguliwa moja kwa moja na kupangwa na OR-TAMISEMI kwenye vyuo vya Serikali. Gharama hizi zitalipwa moja kwa moja NACTVET wakati wa udahili kwenye kumbukumbu namba (Control number) itakayotolewa katika ofisi ya udahili.

3. Mzazi atawajibika kulipa gharama za mafunzo kwa vitendo mwanafunzi atakapokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo nje ya chuo. Gharama hizi zinaweza kujumuisha malazi, chakula, usafiri na gharama zitakazotakiwa kila mwanafunzi kukilipa kituo cha mafunzo kwa vitendo.

**SEHEMU B: MAHITAJI YA MWANAFUNZI AWAPO CHUONI**

Yafuatayo ni mahitaji muhimu ambayo mzazi/mlezi utapaswa kumuandalia mwanafunzi kabla ya kufika chuoni.

## Uniform Zinapatikana Chuoni, Tafadhari Wasiliana Kwa Namba 0712115682

## I. SARE:

**Wasichana:** Magauni mawili (2) meupe ya mikono mifupi na urefu unaopita magoti anapokuwa ameketi; magauni hayo yasiwe na ribbon/urembo. Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni na soksi nyeupe, makoti mawili (2) meupe (mikono mirefu).

**Wavulana**: Suruali mbili (2) za kitambaa cha rangi ya khaki (isiwe "cardet" au "jeans"), mashati mawili yenye rangi nyeupe yenye mikono mifupi na yasiyo na urembo. Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi na soksi nyeupe. Makoti mawili (2) meupe (koti moja liwe na mikono mirefu na lingine mikono mifupi). **NB:** Mara utakapofika chuoni utapewa mwongozo wa mavazi wakati wote uwapo masomoni .

## II. VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA MWANAFUNZI

a) Vitabu vya rejea vya kozi husika utakavyoelekezwa baada ya kufika chuoni.
b) Computer mpakato (laptop) ili kurahisisha kujifunza
c) Flash
d) Vifaa vya kuandikia kwa mfano madaftari, kalamu, rula n.k
e) Nguo na viatu vya michezo mbali mbali.
f) Mwamvuli au koti la mvua
g) Kikokotoo (Calculator)

## III. VIFAA SAIDIZI KWAAJILI YA CHUO

a) 'Ream' mbili (2) ya karatasi (AINA YA DOUBLE A) za kutolea nakala/kurudufu (photocopy) kwa kila muhula kwa wanafunzi wanaoanza na wanaoendelea kila muhula ream moja (1).
b) Pen nataraji box 3 (blue 1, red1 and black 1) kwa ajili ya shughuli mbalimbali chuoni.
c) Hand wash soap 1

Ninakutakia masomo mema.

.........................................................................

**MKUU WA CHUO**

**KIAMBATISHO I: Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Wizara ya Afya**

**Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Wataalam**

**Fomu ya Uthibitisho wa Utii wa Sheria na Taratibu za Chuo kwa Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo ya Afya kwa ngazi za Astashahada na Stashahada**

**Jina la Chuo: ………………………………………………………… Mwaka wa Masomo: …………………………………………………..**

**Kozi: …………………………………………………………………**

**SEHEMU A: SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO**

1. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa katika mazingira ya shule ifikapo saa 2.00 usiku kwa siku za kawaida na saa 4.00 usiku siku za mwisho wa wiki na sikukuu (Jumamosi na Jumapili). Mwanafunzi atakayekuwa nje ya chuo zaidi ya muda uliotajwa hapo juu kwa sababu maalum anatakiwa kupata ruhusa maalum kwa maandishi (gate pass) toka kwa Mkuu wa chuo au Mlezi wa chuo.
2. Kila mwanafunzi atawajibika kwa usafi wa chumba anachoishi na usafi wa mazingira ya chuo.
3. Hairuhusiwi kubandika magazeti/vipande vya magazeti au picha kwenye kuta za majengo ya chuo.
4. Kila mwanafunzi atatakiwa kushiriki kikamilifu katika michezo na shughuli nyingine za chuo kama zitakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
5. Wageni hawaruhusiwi kuingia kwenye eneo la chuo bila idhini ya mlezi au Mkuu wa Chuo. Endapo mgeni/wageni watahitaji kuzunguka na kuangalia maeneo ya chuo, watatakiwa kupata kibali toka kwa Mkuu wa chuo.

6. Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi wakati wa masomo na wanatakiwa kuwa wameondoka kwenye maeneo ya chuo ifikapo saa 12 jioni
7. **Wageni wanatakiwa kuandikisha katika kitabu cha wageni, kinachoonesha jina la mgeni, mahali anakotoka, uhusiano na mwanafunzi anayemtembelea, anuani yake na muda wa kuingia na kutoka.**
8. Hairuhusiwi wanafunzi wa kiume kwenda kwenye vyumba vya kulala wanafunzi wa kike na vivyo hivyo kwa wanafunzi wa kike kwenda kwenye vyumba vya kulala wanafunzi wa kiume.
9. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare za chuo zenye staha wakati wote wanapokuwa darasani, katika mafunzo kwa vitendo hospitalini na shughuli nyingine za chuo kama itakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
10. Matumizi ya pombe, Sigara, madawa ya kulevya hayaruhusiwi mwanafunzi anapokuwa masomoni. Mwanafunzi atakayebainika kutumia atakuwa amevunja sheria na hivyo kuchukuliwa hatua.
11. Upigaji wa kelele katika maeneo ya chuo au hospitali hauruhusiwi.
12. Wanafunzi wote wanawajibika kutunza vifaa na majengo ya chuo. Ni marufuku kujihusisha na uharibifu wa aina yeyote. Aidha, mwanafunzi atakayeharibu mali ya chuo, atawajibika kuilipa pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.
13. Hairuhusiwi kukaa na silaha ya aina yeyote, ikiwemo kisu au panga.
14. Mwanafunzi yeyote mwenye vifaa vya umeme mdogo kama kompyuta, radio ndogo na pasi, atoe taarifa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo. Aidha, mwanafunzi haruhusiwi kuwa na jiko la aina yoyote au kifaa chochote cha kuchemshia maji (heater) katika eneo la chuo.
15. Mwanafunzi anayeumwa anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo. Kila mwanafunzi anayehudhuria matibabu awe na ‘sick-sheet’ kabla ya kupata matibabu. Isipokuwa pale tu matibabu yake yanakuwa ya dharura na upatikanaji wa ‘sick-sheet’ ni mgumu. Hata hivyo, bado mwanafunzi huyo atatakiwa kujaziwa ‘sick-sheet’ baada ya matibabu. ‘Sick-sheet’ zote zinatakiwa kurudishwa kwa Mkuu/Mlezi wa chuo na kutunzwa kwenye majalada ya kumbukumbu za wanafunzi husika.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki katika kutenda makosa ya jinai. Aidha, mwanafunzi yeyote atakayethibitika kushiriki kutenda kosa ya jinai atasitishwa masomo na kuamuriwa kuondoka eneo la chuo haraka iwezekanavyo.
17. Mwanafunzi anatakiwa kushiriki kikamilifu katika matukio yote yanayohusu mafunzo bila kukosa. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuondoka eneo la chuo/mafunzo bila taarifa ya maandishi kutoka kwa mkuu wa chuo/mlezi wa wanafunzi.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha ya matusi au udhalilishaji, kupigana, kufanya migomo, kuandamana kinyume cha utaratibu, kuiba na kumiliki mali kinyume cha sheria.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya vitendo vyenye kushawishi ngono ndani ya mazingira ya chuo na hospitali
20. Mwanafunzi anaruhusiwa kushiriki hafla za kiimani zinazohusiana na imani ya dini mbalimbali baada ya kuwa amepata kibali kutoka kwa mkuu wa chuo. Aidha, ushiriki wa shughuli yoyote ya kidini itakayothibitika kuingilia ratiba ya mafunzo au uvunjifu wa amani hautaruhusiwa.
21. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki au kuendesha harakati za kisiasa chuoni
22. Mwanafunzi atakayedhihirika kuwa na mimba au amempa mwanafunzi mwenzie mimba basi atarudishwa nyumbani kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

23. Mwanafunzi anatakiwa kufuata taratibu zote wakati wa mitihani. Aidha kushiriki katika kugushi matokeo ya mitihani, nyaraka za Serikali hakutavumiliwa, na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

## SEHEMU B: MWONGOZO WA MAVAZI

### 1. NGUO ZINAZORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na pia ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa nguo zinazoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

#### *1.1 Kwa wasichana/wanawake*

a) Wavae sketi au gauni isiyo ya kubana, kitambaa kisichokuwa *transparent* na iwe ndefu ya kuvuka magoti akiwa amekaa
b) Kuvaa sare pamoja na vitambulisho wakati wote wa darasa, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo
c) Sare:
   - Sare kwa kada za vyuo vya Sayansi Shirikishi: Gauni nyeupe ya mikono mifupi isiyokuwa na ribbon
d) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)
e) Nguo safi na zilizopigwa pasi
f) Nguo za michezo na tisheti zilizochaguliwa na taasisi/ Serikali ya wanafunzi
g) Uvaaji wa soksi ndefu za aina moja zenye rangi nyeupe
h) Hijabu iwe ya rangi nyeupe na iwe fupi inayoingizwa kwenye sare

#### *1.2 Kwa wavulana/wanaume*

a) Kuvaa suruali ndefu zisizo za kubana na kuchomekea na kufunga mkanda pamoja na kuvaa vitambulisho wakati wote wa darasani, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo nje ya chuo
b) Sare:
   - Sare kwa kada za vyuo vya Sayansi Shirikishi: Suruali ya khaki na shati lenye mikono mifupi.
c) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)
d) Nguo safi zilizopigwa pasi
e) Nguo zinazoendana na rangi iliyochaguliwa na taasisi/Baraza la taaluma
f) Nguo zenye mtindo wa kushona uliopitishwa na taasisi/Baraza la taaluma
g) Nguo za michezo na tisheti zilizochaguliwa na taasisi/ Serikali ya wanafunzi
h) Uvaaji wa soksi za aina moja zenye rangi nyeupe
i) Vest au T-Shirt inayovaliwa ndani ya shati iwe yenye rangi nyeupe

#### 1.3 Nguo za kujikinga na baridi zinazoruhusiwa kwa jinsia zote

*a)* Sweta lenye rangi nyeupe lisilokuwa na urembo au maandishi yeyote.

b) Kwa vyuo vilivyoko kwenye mikoa yenye baridi kali wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa mavazi ya nyongeza juu ya sare ya chuo mfano skafu nyeupe na koti lenye rangi nyeupe

## 2. NYWELE ZINAZORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na pia ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa mitindo ya nywele inayoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

### *2.1 Kwa wasischana/wanawake*

a) Nywele fupi za asili za kuchania kitana
b) Nywele ndefu za asili zifungwe kwa vibanio kuelekea kisogoni ili sura ionekane na zisiachwe kuning'inia
c) Nywele za asili za kusuka kwa msitari bila rasta (*Utii wa Rhoda*)

### *2.2 Kwa wavulana/ wanaume*

a) Nywele fupi za asili zinazolingana za kuchania kitana

## 3. UREMBO UNAORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa aina ya urembo unaoruhusiwa ni kama ifuatavyo: a) Pete za ndoa b) Kucha fupi

c) Saa
d) Miwani kwa wenye matatizo ya macho
e) Kofia kwa wenye matatizo ya ngozi (Albino)

## 4. VIATU VINAVYORUHUSIWA

Ili kurahisisha usimamizi wa mwongozo huu vyuoni na ili kuwasaidia wanafunzi waweze kufanya kilicho sahihi, ufafanuzi wa viatu vinavyoruhusiwa ni kama ifuatavyo:

a) Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni.
b) Viatu vya michezo wakati wa michezo

## 5. MAVAZI YASIYORUHUSIWA

### 5.1 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wasichana/ wanawake

a) Nguo zinazobana
b) Nguo (gauni/sketi) fupi zinazoacha magoti wazi
c) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua
d) Nguo zinazoonyesha maungo/ nguo za ndani (transparent)
e) Nguo zilizokunjamana (Hazikunyooshwa)
f) Nguo chafu (Hazikufuliwa)
g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo
h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
j) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za Serikali

k) Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi
l) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) kwenye sehemu ya magoti na mapajani
m) Kwenda na khanga/kitenge kwenye bwalo la chakula bila kuwa na nguo ya ndani
n) Kuvaa nguo za kulalia (night dress) kwenye makundi ya kusoma na kupita nazo kwenye mazingira ya chuo
o) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani
p) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma
q) T-shirt zenye picha za kutisha na maandishi yasiyo na staha

**5.2 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wavulana/wanaume**

a) Suruali aina ya kadeti au jeans kutumika kama sare (hata kama ni ya rangi ya khaki) b) Suruali za kubana (modo)
c) Shati la kubana (Slimfit)
d) Kuvaa suruali mlegezo (*Kata K*)
e) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua
f) Kufunga vifungo vichache vya shati ili kifua kionekane
g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo
h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
j) Suruali yoyote fupi au iliyoachwa bila kupindwa chini
k) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) kwenye sehemu ya magoti na mapajani
l) Kaptura ya aina yoyote
m) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani
n) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma
o) T-shirt zenye picha za kutisha na maandishi yasiyo na staha.

**6. NYWELE ZISIZORUHUSIWA**

a) Nywele chafu ambazo hazikutengenezwa vizuri
b) Nywele bandia au zilizopakwa rangi
c) Kufuga nywele ndefu kwa wavulana/wanaume
d) Kusuka rasta ndefu au mtindo wowote wa nywele za kuning'inia
e) Unyoaji nywele mitindo isiyofaa k.m *kiduku, pank*, *zungu la unga* (kipara) f) Kufuga ndevu
g) Kunyoa ndevu kwa mitindo isiyofaa k.m mzuzu, *timberland au kufuga ndevu* n.k

**7. UREMBO USIORUHUSIWA**

a) Hereni, Bangili, Mikufu, Pete ambazo si za ndoa pamoja na manukato yenye harufu kali b) Kunyoa nyusi na kupaka wanja c) Kupaka rangi za midomo
d) Kufuga kucha ndefu na upakaji rangi kwenye kucha
e) Uvaaji wa kucha bandia
f) Meno ya urembo wa dhahabu hayaruhusiwi

**8. VIATU VISIVYORUHUSIWA**

a) Kandambili pamoja na makobazi
b) Viatu vya michezo pamoja na raba (isipokuwa wakati wa shughuli maalum za michezo)
c) Viatu vya rangi isiyopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni
d) Kuvaa viatu bila socks
e) Viatu vya mchuchumio
f) Viatu vya kisigino vyenye kutoa sauti kwenye sakafu
g) Kufuga ndevu

**ANGALIZO:** Uvunjaji wa taratibu zilizoainishwa hapa juu unaendana na adhabu, ambazo zimeelekezwa katika kitabu cha maadili ya wanafunzi walioko katika vyuo vya afya kilichotolewa, na wizara ya afya mwaka 2019 (Disciplinary Code for Students in Health Training Institutions Revised 2019)

**SEHEMU C: UTHIBITISHO**

Mimi ......................................................................niliyechaguliwa kujiunga na masomo ya Afya kwa kada ya……………………………………. Ngazi ya ………………………………………………..
nathibitisha kuzisoma na kuzielewa Sheria na Taratibu za Chuo pamoja na Mwongozo wa Mavazi niwapo chuoni.
Hivyo nathibitisha kuwa nitakuwa tayari kuzifuata kwa kipindi chote nitakachokuwa hapa chuoni na nakubali kuchukuliwa hatua za kinidhamu endapo nitathibitika kukiuka taratatibu hizo.

Jina la Mwanafunzi: …………………………………………………………………

Sahihi: ………………………………………………………………………………….

Tarehe: ………………………………………………………………………………

Jina la Mzazi/Mlezi: …………………………………………………………………

Sahihi: ………………………………………………………………………………….

Tarehe: ………………………………………………………………………………

Imepokelewa na kushuhudiwa na:

Jina la Mkuu wa Chuo: …………………………………………………………………

Sahihi: …………………………………………………………………………………..

Tarehe: ……………………………………………

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HEALTH**

**MEDICAL EXAMINATION FORM FOR STUDENTS JOINING ALLIED HEALTH TRAINING INSTITUTIONS AND NURSING SCHOOLS**

**NAME OF THE INSTITUTION: ……………………………………………………………**

**PROGRAMME: ………………………………………………………………………….**

**YEAR OF STUDY: ……………………………………………………………………**

**PART A: STUDENT'S PARTICULARS**

STUDENT'S FULL NAME: ………………………………………………………………..

DATE OF BIRTH: ……………………………………………………………………….

SEX: (Male/Female)………………………MARITAL STATUS: ……………………………..

**PART B: STUDENT'S MEDICAL HISTORY**

Does the examinee have current history of any of the following? Indicate ***YES*** or ***NO***

Tuberculosis? ...............................

Epilepsy? .....................................

Sickle cell? ………………………

Asthmatic or with Allergic to something (*specify*)? …………..

Psychiatric? ……………………… Vision

impairment? ……………..

Hearing disorder? ……………….

Physical disability? ……………..

Any other significant medical condition/disorder? (*please specify*) …………………………

## PART C: PHYSICAL EXAMINATION

Height (cm): ……………………. Weight (kg): ………………….. BP (mmHg): ………………..

Any significant finding from systemic examinations (*please specify*):

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

## PART D: INVESTIGATIONS' FINDINGS

Please indicate any significant finding from the following Laboratory and Radiological tests

FBP: …………………………………….. Urinalysis: ………………………………………………

Random Blood Sugar (*provide the results*): ………………………… Blood group ……………….

Stool analysis: ………………………………

Any other relevant investigation performed (*please give brief findings*):

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

## PART E: CONCLUSION

I have examined Mr./Miss/Mrs… ............................................................................................... and Consider that he/she is physically and mentally **fit/not fit** to be admitted to the college for studies.

…………………... ...………… ……………………………………..

Name Signature Date

Qualification ……………………… Title ……………………………………….

Hospital's Name: ………………………………………………………………………………..

(*Official hospital's stamp*)

<u>**KIAMBATISHO III: Fomu ya Usajili**</u>

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF HEALTH**

**INSTITUTION NAME: ……………………………………………………………….**

**STUDENT'S REGISTRATION FORM**

**ADMISSION OFFICE**

STUDENT NAME ……………………………………………………………

DATE OF BIRTH …………………………………………………………….

NATIONALITY ………………………………………………………...

ADDRESS …………………………………………………………………

SEX Male: ☐ Female: ☐

MARITAL STATUS ………………………………………………………

TELEPHONE NUMBER …………………………………………………

NACTVET REG NUMBER ………………………………………………

PROGRAM ………………………………………………………………….

NTA LEVEL ………………………………………………………………

REMARKS FROM NACTVET SYSTEM Available: ☐ Not Available: ☐

*If **Not Available**, state why?*

………………………………………………………………………………………..…….

ADMISSION OFFICER'S SIGNATURE ……………………………………………

## TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

**NDUGU WA KWANZA**

JINA KAMILI (MATATU) ……………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………… ………………………………………

ANUANI YA POSTA: ……………………………………………………………

MTAA: ……………………………KATA: ………………...WILAYA: ………….

MKOA: ……………………………………………NAMBA YA SIMU: ……………

BARUA PEPE: ………………………………………….

Passport size

**NDUGU WA PILI**

JINA KAMILI (MATATU) ……………………………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………… ………………………………………………………...

ANUANI YA POSTA: ………………………………………………………………………………

MTAA: ……………………………KATA: ………………...WILAYA: …………………...

MKOA: ……………………………………………NAMBA YA SIMU: ……………………

BARUA PEPE: ………………………………………….

Nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi na kweli tupu.

JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI………………………..……………………………………….

SAHIHI: …………………………………………. TAREHE:………………………………………….

Imesainiwa mbele ya (Ijazwe na Mtendaji wa Kata/mtaa/Kijiji)

JINA KAMILI ……………………………………………CHEO: ………………………………………..

ANUANI YA POSTA: ………………...………………………………………………………..

MTAA: ……………………………KATA: ………………..WILAYA: ……………………..

MKOA: ……………………………………………NAMBA YA SIMU: ………………………..

SAHIHI: ……………………………… MUHURI WA OFISI: ………………………………

TAREHE: …………………………………………………….

**ACCOUNTANT'S OFFICE *(Payment of School Fees)***

TOTAL AMOUNT NOT PAID ….…………………………………………..

REASON FOR AMOUNT NOT PAID ………………………………….…………………..

………………………………………..………………………………………………

………………………………………..……………………………………….…….

PAID SMESTER II EXAMINATION FEES? **YES** ☐ **NO** ☐

ACCOUNTANT'S SIGNATURE ……………………………………………..

STUDENT'S SIGNATURE ……………………………………………..

**PATRON / MATRON OFFICE (*if accommodation offered*)**

HOSTEL NAME / BLOCK ……………………………………………..

ASSIGNED ROOM NUMBER ……………………………………………..

STUDENT'S DISABILITY (*Briefly describe in case of any disability*)

………………………………………..……………………………………………..

………………………………………..……………………………………………..

………………………………………..……………………………………………..

PATRON / MATRON SIGNATURE ……………………………………………..

**STUDENT'S DECLARATION**

I ........................................................................ declares that all the information provided are correct to the best of my knowledge and shall be held responsible in case of wrong information.

STUDENT'S SIGNATURE ……………………………………………..

DATE ……………………………………………..

**WIZARA YA AFYA**

**KIAMBATISHO NA. IV: FOMU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. **Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi**

Mimi Bw./Bi/……………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa Bw./Bi……………………………………………………..…nakiri kupokea maelekezo ya Wizara/Chuo yanayomhusu kijana wangu. Ninaahidi kumsimamia mwanafunzi huyu atekeleze maelekezo yote ikiwa ni pamoja na kulipa ada kwa ukamilifu ili aweze kupokelewa chuoni na kuanza masomo ndani ya muda uliopangwa. Pia ninaahidi kushirikiana na uongozi wa chuo kuhakikisha mwanafunzi huyu anasoma kwa bidii na kuonyesha nidhamu wakati wote wa mafunzo.

Jina kamili la mzazi/mlezi (Wa kiume)…………………………………………………

Kazi anayofanya: ………………………………………………………………

Anuani kamili: ………………………………………………………………

Namba za simu: ………………………………………………………………

Barua pepe: ………………………………………………………………

Saini: ………………………………………………………………

WEKA PICHA YA BABA MZAZI/ MLEZI WA KIUME HAPA

Jina kamili la mzazi/mlezi (Wa kike)……………………………………………………….

Kazi anayofanya: ……………………………………………………………….

Anuani kamili: ……………………………………………………………….

Namba za simu: ……………………………………………………………….

Barua pepe: ……………………………………………………………….

Saini: ……………………………………………………………….

WEKA PICHA YA BABA MZAZI/ MLEZI WA KIUME HAPA

**Taarifa ya Mtendaji wa kata**

**Jina la Afisa Mtendaji wa Kata:** ………………..…………………………….……………..

**Jina la kata:** ……………….…………………….…………………………………..

**Anuani :** ……………………………………………………………………………….

**Namba za simu:** ……………………………………………………………………………….

**Barua pepe:** ……………………………………………………………………………….

**Saini**: ……………………………………………………………………………….

Muhuri wa ofisi